**FORM PLUPA L-1** **(r.9)**

# SERIKALI YA KAUNTI YA NYERI

## IDARA YA ARDHI, MIPANGO YA USTAWI NA USTAWISHAJI WA MIJI

# ILANI YA NIA YA KUTAYARISHA MIPANGO YA KIENEO YA USTAWISHAJI NA MATUZI YA ARDHI

| S.No | Jina la Mpango wa Ustawishaji | Eneo |
|---|---|---|
| 1 | Mpango wa Kieneo wa Ustawi na Matumizi ya Ardhi katika Kijiji cha Muthuthini. | Kaunti-ndogo ya Mukurweini |
| 2 | Mpango wa Kieneo wa Ustawi na Matumizi ya Ardhi katika eneo la Karatina Mjini | Kaunti-ndogo ya Mathira East |
| 3 | Mpango wa Kieneo wa Ustawi na Matumizi ya Ardhi katika eneo la Othaya Mjini | Kaunti-ndogo ya Othaya |
| 4 | Mpango wa Kieneo wa Ustawi na Matumizi ya Ardhi katika eneo la Chaka Mjini | Kaunti-ndogo ya Kieni East |
| 5 | Uhakiki wa Mpango Jumuishi wa Kimkakati wa Ustawishaji wa Mji wa Nyeri (2014-2034) | Kaunti-ndogo ya Nyeri Central |

Kwa mujibu wa kanuni za Sehemu ya 47 ya Sheria ya Mipango ya Ustawishaji na Matumizi ya Ardhi, 2019, ILANI inatolewa hapa kwamba Serikali ya Kaunti ya Nyeri inakusudia kuanza maandalizi ya mipango iliyotajwa hapo juu tarehe **16 Machi 2026.** Madhumuni ya mipango hii ni kuelekeza shughuli za ustawishaji katika maeneo husika ya mijini kwa njia jumuishi ili kuwezesha ustawishaji endelevu na kutoa msingi wa kufanikisha miundomsingi na vifaa vya umma.

Malengo ya mipango ya Kieneo wa Ustawi na Matumizi ya miji ya kipindi cha miaka kumi (10) ni:

a) Kutambua changamoto za kimaendeleo zinazokabili maeneo husika ya na kubaini mikakati ya kuzisuluhisha;
b) Kukuza matumizi ya ardhi na rasilimali, kwa uwiano, ufanisi an usawa;
c) Kutoa mwongozo wa kuelekeza na kuratibu uboreshaji, ufanikishaji na matengenezo ya miundomsingi;
d) Kulinda na kuhifadhi mazingira asilia;
e) Kuhimiza ushiriki wa wadau katika ustawishaji kwa mbinu shirikishi;
f) Kuweka msingi wa upimaji na udhibiti wa viwanja na huduma za umma;
g) Kuunda msingi wa usimamizi wa matumizi ya ardhi na udhibiti wa shughuli za ustawishaji.

Shughuli hii ni shirikishi hivyo basi wadau wote wanaalikwa kushiriki. Maoni, maswali au mapendekezo kuhusu suala hili wanaweza kuyatuma kwa maandishi katika muda usiozidi siku **ishirini na moja (21)** kuanzia siku ya kuchapishwa kwa ilani hii :

**Waziri wa Kaunti,**
**Idara ya Ardhi, Mipango ya Ustawi na Ustawishaji wa Miji**
**Serikali ya Kaunti ya Nyeri**
**S.L.P 1112-10100, Nyeri au** lands@nyeri.go.ke

**Tarehe: 5 Februari 2026**

**MHE. NDIRANGU GACHUNIA**
**WAZIRI WA KAUNTI (CECM)**
**IDARA YA ARDHI, MIPANGO YA USTAWI NA USTAWISHAJI WA MIJI**